## TUME YA RAIS YA KUCHUNGUZA MATUKIO YA UVUNJIFU WA AMANI YALIYOTOKEA WAKATI NA BAADA YA UCHAGUZI MKUU WA OKTOBA, 2025

### HADIDU ZA REJEA

Katika kutekeleza majukumu yake Tume itaongozwa na Hadidu za Rejea zifuatazo:

1. Kuchunguza na kubainisha chanzo halisi cha ghasia zilizotokea wakati wa Uchuguzi Mkuu nchini uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025 na siku chache zilizofuata;

2. Kuchunguza lengo kuu lililokusudiwa na waliohusika katika kupanga na kutekeleza vitendo hivyo vya ghasia na uvunjifu wa amani;

3. Kuchunguza na kubainisha madhara yaliyojitokeza kutokana na ghasia hizo ikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na miundombinu na madhara ya kiuchumi na kijamii;

4. Kuchunguza mazingira na hatua zilizochukuliwa katika kubaini na kukabiliana na ghasia zilizojitokeza;

5. Kupendekeza maeneo yanayohitaji kuimarishwa zaidi ili kuongeza uwajibikaji wa viongozi na raia kwenye kulinda amani, utawala wa sheria, haki za binadamu, utawala bora na mfumo madhubuti wa majadiliano ya kisiasa, kijamii na kiuchumi hadi kufikia maridhiano ya kitaifa na kuhakikisha vurugu kama hizi hazitokei tena; na

6. Kuchunguza jambo lolote ambalo Tume itaona kuwa ni muhimu na linaendana na majukumu ya Tume.